Government of Western Australia
Mental Health Commission

### Maelezo kwa Watu Wanaoteuliwa

Kama mtu aliyeteuliwa, wajibu yako ni kumsaidia mtu aliyeteua kwa kuhakikisha haki zake zinatetea, na faida na matakwa yake inafikiriwa wakati huyu ni mgonjwa.

Unakubali kuwa mtu aliyeteuliwa wa mtu kwa kuweka sahihi kwa Fomu 12A.

Kama mtu aliyeteuliwa unastahili kupokea maelezo kuhusu, na kuhusisha katika, mambo yanayohusu matibabu na utunzaji wa mgonjwa. Wafanyakazi atakuwasiliana nawe na maelezo hayo isipokuwa mtaalum wa magonjwa ya akili wa mgonjwa akiamua kwamba kutoa maelezo fulani au kukuhusisha katika mambo fulani sio kwa faida nzuri za mgonjwa.

Unaweza kustaafu kuwa mtu aliyeteuliwa wakati wowote kwa kumwambia mgonjwa kwa maandishi kwamba hutakuwa tena mtu wake aliyeteuliwa na kuweka sahihi kwa hivi. Lazima pia umjulishe mfanyakazi kwamba wewe sio tena mtu aliyeteuliwa.

Kama mtu aliyeteuliwa wewe na mmojawapo wa 'wanaosaidia kibinafsi' wa mgonjwa na una haki sawa na mtunzaji wa mgonjwa au wanafamilia wa karibu wake. Kujifunza zaidi kuhusu haki za wanaosaidia kibinafsi soma brosha inayoitwa 'Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi'.

### Maelezo zaidi

Maelezo katika brosha hii inahusisha masheria ambayo yamo Sheria ya Afya ya Akili 2014. Maelezo kuhusu Sheria hii imefupishwa katika seti ya brosha zifuatazo:

- Kupendekezwa kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi
- Maagizo ya matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa hospitalini
- Maagizo ya matibabu ya jamii
- Maelezo kwa wagonjwa wa hiari
- Kupokea matibabu kwa ugonjwa wa akili
- Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi
- Watu walioteuliwa: Jinsi ya kuteua na maana kwake

Brosha zingine zinapatikana kutoka:

- Baraza ya Afya ya Akili
- Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili
- Kituo cha Sheria ya Afya ya Akili

Kwa maelezo zaidi kuhusu Sheria ya Afya ya Akili 2014 na nyenzo zingine, angalia tovuti ya Tume ya Afya ya Akili: www.mhc.wa.gov.au au pigia simu (08) 6272 1200.

This document can be made available in other languages and alternative formats on request.

Published by the Mental Health Commission (2015)

# Watu walioteuliwa:

# Jinsi ya kuteua na maana kwake



Brosha hii inakupa maelezo kuhusu njia ya kuteua mtu wako aliyeteuliwa na maana yake. Pia inawapa watu walioteuliwa maelezo kuhusu majibu yao na haki zao chini ya Sheria ya Afya ya Akili 2014.

Wajibu ya watunzaji na wanafamilia wa karibu inatambuliwa sana na wana haki kufahamishwa na kuhusisha katika matibabu na utunzaji wa mgonjwa.

Unaweza kuwa na mtu katika maisha yako (kwa mfano rafiki), asiyekuwa mtunzaji wako au mwanafamilia wa karibu, lakini ni muhimu kwa wewe kuwa huyo ana wajibu katika matibabu na utunzaji wako.

Unaweza kuchagua mtu huyo kuwa "mtu aliyeteuliwa" wako na kufanya hivyo vinampa mtu yule wajibu, haki na hali sawa na mtunzaji au mwanafamilia wa karibu.

## Wajibu ya mtu aliyeteuliwa

Wajibu ya mtu wako aliyeteuliwa ni kukusaidia kwa kuhakikisha haki zako zinatetea na faida na matakwa yako inafikiriwa wakati wewe ni mgonjwa.

Kawaida mtu wako aliyeteuliwa atahusisha na matibabu na utunzaji wako pamoja na kufikiri uchunguzi kwa matibabu na utunzaji na kukutoa na msaada.

Mtu wako aliyeteuliwa pia atapewa maelezo kuhusu:

- Ugonjwa wako wa akili, uchunguzi kwa matibabu na utunzaji na jibu lako kwa matibabu yoyote yanayotolewa,
- sababu ambazo zinachangia kwa agizo la matibabu kwa mgonjwa asiyekusudiwa, na
- huduma zinazopatikana kuridhisha mahitaji yako.

Mtu wako aliyeteuliwa hatafahamishwa/ kuhusisha kwa mambo fulani kama mtaalum wako wa magonjwa wa akili anaona sio kwa faida nzuri zako.

## Nani anaweza kuteua?

Mtu yeyote, pamoja na mtoto, anaweza kuteua mtu kuwa mtu wake alieteuliwa. Hata hivyo, lazima uweze kuelewa kuteua ni nini na maana kwake.

## Unaweza kuteua nani?

Unaweza kuomba mtu yeyote unayetaka, kuwa mtu wako aliyeteuliwa. Lazima lakini awe na umri wa miaka 18 au zaidi na kukubali kuteuliwa. Unaweza kuwa mtu aliyeteuliwa mmoja tu kwa wakati moja

## Jinsi ya kuteua

Kuteua, lazima ujaze Fomu 12A – Kuteua mtu aliyeteuliwa. Unaweza kuomba wafanyakazi kwa nakala ya fomu hii, au unaweza kupata nakala kutoka www.mhc.wa.gov.au.

Nyote wewe na mtu wako aliyeteuliwa mweke sahihi zenu na sahihi zote mbili zithibitishwa. Watu ambao wana mamlaka kuwa shahidi ni pamoja na daktari, muuguzi, mfamasi, mwalimu na hakimu wa amani. Orodha nzima inapatikana hapa:

http://www.courts.dotag.wa.gov.au/_files/ Professions_witness_statutory_declarations. pdf

Unahitaji kujulisha huduma zinazokupa matibabu kuhusu kuteua kwako. Mfanyakazi atafanya nakala ya fomu ya kuteua kwako na ataweka kwa kumbukumba lako la uganga.



## Jinsi ya kuteua kumalizika?

1. Unaweza kumaliza kuteua wakati wowote na njia zozote (kwa mfano kwa kuwaambia wafanyakazi kwamba mtu sio tena mtu wako aliyeteuliwa).
2. Unaweza kumaliza kuteua kwa njia ya kuteua mpya mwengine. Lazima ujaze Fomu 12A mpya kufanya hivi.
3. Mtu wako aliyeteuliwa anaweza kustaafu kwa sababu yoyote na afanye kwa njia ya maandishi.
4. Baraza ya Afya ya Akili inaweza kumaliza kuteua kama ikiamua mtu aliyeteuliwa hawezi kufanya wajibu ile, au anakudhara kwako.